



CATHOLIC DIOCESE OF MOSHI

ST. PAMACHIUS INCLUSIVE SECONDARY SCHOOL

P. O. BOX 1303

MOSHI – TANZANIA

st.pamachusinclusive2019@gmail.com

MAELEZO MUHIMU KUHUSU SHULE

A. UTANGULIZI

Shule ya Sekondari St. Pamachus Inclusive ni mojawapo ya Shule zinazomilikiwa na kusimamiwa na Jimbo Katoliki Moshi.

Shule iko katika Kijiji cha Kimashuku, Kata ya Mnadani, Wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro. Shule ipo umbali wa kilomita moja na nusu kutoka barabara kuu ya Moshi-Arusha, kutokea kituo cha mabasi cha Mnadani. Kufika shuleni, ukitokea Moshi mjini, panda basi linalokwenda Sanya Juu au Machame, shukia kituo cha Mnadani. Kwa anayetokea upande wa Arusha au Bomang'ombe, shukia kituo hicho hicho cha Mnadani. Usafiri wa kutoka kituoni kufika Shuleni upo hapo hapo kituoni.

Shule ya Sekondari St. Pamachus Inclusive ni Shule Jumuishi; yaani, inayotoa elimu ya sekondari kwa Watoto Wenye Mahitaji Maalum na wasiokuwa na Mahitaji Maalum kwa pamoja. Mazingira ya shule yanatengenezwa hivyo kwamba watoto wote – wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum – wanaweza kutumia miundombinu yote ya shule kwa uhuru. Shule inalenga ufaulu katika viwango vya juu kwa kila mwanafunzi. Hivyo walimu, vifaa vya kujifunzia na mazingira ya kujifunzia yameandaliwa kumuwezesha mwanafunzi kufikia ufaulu wa hali ya juu, akijiandaa kufikia malengo yake kimaisha.

Shule ya Sekondari St. Pamachus Inclusive ni ya bweni kwa wavulana na wasichana, wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum, kidato cha kwanza hadi cha nne.

Sekondari yetu inatoa elimu kwa mujibu wa mitaala iliyoidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikitilia mkazo malezi bora kwa wanafunzi, uchaji, nidhamu, taaluma na maadili katika nyanja zote za maisha. Masomo yatakayofundishwa ni ya Sayansi, Biashara na Sanaa.

B. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Siku ya kufungua shule ni tarehe -----; kuanzia saa tatu kamili asubuhi (3:00) hadi saa sita na nusu (6:30) mchana.
2. Siku ya kuwasili Mwanafunzi asindikizwe na Mzazi/Mlezi.
3. Mwanafunzi afike na cheti chake cha kuzaliwa kilichotolewa serikalini.
4. **Malipo yote ya fedha za shule yafanyike Benki kuanzia JANUARI 1.** Mzazi / Mlezi afike shuleni akiwa

na 'Pay In Slip' za Benki. Hatupokei fedha taslimu shuleni!

5. Mzazi / Mlezi atawajibika kumpatia mwanafunzi fedha kiasi kwa ajili ya mahitaji binafsi wakati akiwa shuleni. Fedha hizi zitakabidhiwa kwa Mhazini wa Shule kwa usalama. Mwanafunzi atapewa fedha kadiri ya mahitaji / maelekezo ya mzazi wakati wote.
6. Mzazi/Mlezi ahakikishe mwanafunzi ana vifaa ulivyoandikiwa kununua na kuvileta. Vifaa vinavyopatikana Shuleni atakabidhiwa mara ukishapokelewa shuleni.
7. Fika naFomu iliyojazwa na Daktari”, “Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi”, Ahadi ya mzazi” na “Fomu ya kukubali masharti ya shule zikiwa zimejazwa kwa usahihi.

C. ADA YA SHULE

Ada ya Shule kwa Mwaka (ilipwe kwa mkupuo au kwa kila miezi sita)

1,800,000/-

D. VITU VINAVYOPATIKANA SHULENI KWA KULIPIA (SARE NA VIFAA VYA MATUMIZI SHULENI)

Na.	Maelezo	Idadi	Gharama	Mvulana	Msichana
1	Sketi (Wasichana tu)	2	20,000.00		40,000.00
2	Suruali (Wavulana tu)	2	20,000.00	40,000.00	
3	Mashati ya mikono mifupi (Wote)	2	10,000.00	20,000.00	20,000.00
4	Tai	2	10,000.00	20,000.00	20,000.00
5	Soksi ndefu sizizo na urembo	4	4,000.00	16,000.00	16,000.00
6	T-shirt ya kijivu (ya kuvalia ndani ya Truck suit)	2	7,000.00	14,000.00	14,000.00
7	Sweta	2	20,000.00	40,000.00	40,000.00
8	Nguo za kushindia (Truck Suit) Wote	2	25,000.00	50,000.00	50,000.00
9	Nguo za Michezo Truck suit (Was.)	1	25,000.00		25,000.00
10	Nguo za Michezo –bukta & T-shirt (Wav)	1	18,000.00	18,000.00	
11	Godoro (linalipiwa kwa mwaka)	1	5,000.00	5,000.00	5,000.00
12	Shuka mpya	2	18,000.00	36,000.00	36,000.00
13	Mto wa kulalia	1	10,000.00	10,000.00	10,000.00
14	Foronya za mto	2	6,000.00	12,000.00	12,000.00
15	Chandarua	1	12,000.00	12,000.00	12,000.00
16	Vyombo vya kulia	1	15,000.00	15,000.00	15,000.00
17	Noo ya kuogea	1	10,000.00	10,000.00	10,000.00
				318,000.00	325,000.00

E. Vitu Anavyopaswa Kuvileta Anapokuja Shuleni

Vifaa hivi ni kwa ajili ya matumizi ya darasani na matumizi binafsi ya mwanafunzi. Kila mwanafunzi atakaguliwa kuhakikisha ana vifaa vyote kabla ya kupokelewa shuleni. Kiasi kilichooneswa hapa ni makisio

ya sisi walezi. Mzazi anaweza kuongeza kadiri anavyoona inafaa.

Na.	MAHITAJI	KIASI	MAELEKEZO
1	Daftari 'Counter Book' 3Q	14	Ajenazo
2	Daftari Ndogo (Msomi)	14	Ajenazo
3	Kalamu bluu au nyeusi (za kutosha)	10	Ajenazo
4	'Mathematical Set' (Kompasi)	1	Ajenayo
5	Rula	1	Ajenayo
6	Penseli (za kutosha)	5	Ajenazo
7	Kichonge	1	Ajenacho
8	Kifutio	3	Ajenacho
9	Kamusi ya Kiswahili Sanifu	1	Ajenayo
10	Dictionary (Oxford Advanced Learner's Dictionary)	1	Ajenayo
11	Karatasi nyeupe zisizo na mistari (Plain Paper A4)	Rim 1	Ajenazo
12	Mkanda mweusi (wavulana tu)	1	Ajenao
13	Viatu vyeusi vya ngozi, vyenye kamba, vinavyofunika miguu	Pea 2	Ajenavyo
14	Viatu vya michezo	Pea 2	Ajenavyo
15	Taulo kubwa	2	Ajenazo
16	Tochi (kwa tahadhari)	1	Ajenayo
17	Kandambili	Pea 2	Ajenazo
18	Toilet Papers	9 au zaidi	Ajenazo
19	Rangi nyeusi ya Viatu (ya kutosha)	Kopo 3	Ajenazo
20	Brashi ya kupaka rangi kwenye viatu	1	Ajenazo
21	Brashi ya kung'arishia viatu	1	Ajenayo
22	Sabuni ya kufulia ya mche	Miche 3	Ajenayo
23	Sabuni za kuogea	6	Ajenazo
24	Dawa ya kuswaka (kubwa)	3	Ajenayo
25	Miswaki	3	Ajenayo
26	Mafuta ya kujipaka (kopo kubwa)	2	Ajenayo
27	Kitana	1	Ajenacho
28	Saa ya mkononi	1	Ajenayo
29	Nguo za ndani za kutosha		Ajenazo
30	Taulo za kike (kwa wasichana)	7 (walao)	Ajenazo
31	Sanduku la bati (kubwa kadiri)	1	Ajenalo
32	Picha - passport size	2	Ajenazo
33	Kofuli ndogo	2	Ajenazo
34	Shavers (kadiri ya mahitaji ya mtoto)	6	Ajenazo
35	Soksi ndefu za michezo	Pea 2	Ajenazo

36	Kofia pana ya kuzuia jua (kwa wenye Ualbino)	Walao 2	Ajenazo
37	Nguo za shule alikosoma (kwa ajili ya siku za mwanzo tu!)	2	Ajenazo
38	Nguo mbili za heshima za kushindia (kwa muda tu)	2	Ajenazo
39	Fedha ya mfukoni (Poket money)	30,000/-	Ajenazo

F. Kwa Wanafunzi:

1. Hapa shuleni hairuhusiwi kusuka nywele, kufuga ndevu, kufuga kucha, kuchora tatoon, au kuvaa herein. Hivyo haturuhusu yeyote aje akiwa katika hali hizi!
2. Mzazi/Mlezi anapaswa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Shule kuhusu mavazi ambayo hayajatajwa hapo juu, na ambayo mwanae anapaswa kuyatumia kwa sababu za kiafya.

G. Maelekezo Muhimu Kuhusu Ulipaji wa Fedha

1. Malipo yote ya mwanafunzi yafanyike kupitia Benki. Hatupokea fedha taslimu shuleni.

2. **Malipo yote ya Ada (sehemu C)** yalipwe kwenye Akaunti:

Jina la Akaunti: 'St. Pamachus Inclusive Secondary School - Fees'

Namba ya Akaunti: 00511503575303

Benki: Mkombozi Commercial Bank

Tawi: Moshi

3. **Malipo mengine yote (sehemu D)** yalipwe kwenye akaunti:

Jina la Akaunti: "St. Pamachus Inclusive Secondary School – Others"

Namba ya Akaunti: 00511503575304

Benki: Mkombozi Commercial Bank

Tawi: Moshi